

UTANGULIZI

Halmashauri ya Mji wa Kibaha ni miongoni mwa Halmashauri 9 za Mkoa wa Pwani ambayo ilianzishwa tarehe 17 Septemba, 2004 kwa Sheria Na. 7 na 8 ya Mwaka 1982 kifungu kidogo cha 8 na 9 cha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Miji/Mamlaka za Wilaya) kwa kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN No.352) la tarehe 19/04/2004 na hati ya kuanzishwa kwake iliyosainiwa na Katibu wa Bunge tarehe 17 Oktoba, 2007

Halmashauri ya Mji Kibaha kama zilivyo halmashauri nyingine ipo chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hata hivyo mamlaka ya uendeshaji wa shughuli za Kila siku zimewekwa chini ya madiwani 19 kati yao, Madiwani 14 ni wawakilishi wa Wananchi kutoka kwenye kata na Madiwani 5 wa Viti maalum.Wote hupatikana ama kwa kuchaguliwa au kwa kuteuliwa kwa mujibu wa Kifungu kidogo cha 19 cha sharia. Kwa ujumla shughuli za utendaji na utekelezaji wa majukumu ya kila siku yapo chini ya Mkurugenzi wa Mji.

MAHALI

Halmashauri ya Mji wa Kibaha ipo Km.40 kutoka jiji la Dar-es-Salaam. Aidha, inapakana Manispaa ya Ubungo upande wa Mashariki, Bagamoyo Kaskazini, Kisarawe upande wa Kusini na Mji mdogo wa Mlandizi upande wa Magharibi. Ni miongoni mwa halmashauri tisa (9) zilizopo kisheria kwenye Mkoa wa Pwani. Halmashauri ya Mji Kibaha ipo kati ya latitudo 6.8° Kusini na longitude 38.2° na 38.5° Mashariki na inaunganishwa na Bagamoyo mjini kwa barabara zinazopitika muda wote.

HALI YA HEWA

Halmashauri ya Mji Kibaha hupata hali ya hewa ya Joto kubwa Kipindi cha Mwezi Desemba, na baridi kipindi cha Mwezi Julai kila Mwaka.Aidha, Halmashauri ya Mji Kibaha hupata Mvua za wastani ,hata hivyo baadhi ya maeneo hupata mvua kidogo.Kwa Miaka Mitano mfululizo ,Halmashauri ya Mji Kibaha imepata mvua Kidogo isiyozidu Wastani wa mm 700

IDADI YA WATU

Halmashauri ya Mji Kibaha, kutokana na takwimu ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Inakadiriwa kuwa na idadi ya watu 128,488 kati yao Wanawake ni 65,835 na Wanaume ni 62,653 kukiwa na kaya 17.788 na wastani wa watu 4.1 kwenye kila kaya.

49% ya wakazi wa Mji wa Kibaha ni wanaume wakati wanawake ni 51% (Kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya 2012).Wastani wa Jumla wanaume 95 dhidi ya 100 ya wanawake.Kwa sasa Halmashauri ya Mji Kibaha inakadiriwa kuwa na idadi ya wakazi144,241 kati yao 70,334 ni wanaume na wanawake 73,906.

Makabila makuu yanayopatikana kwenye Mji wa Kibaha ni Wazaramo, Wamatumbi na Wangindo, hata hivyo kutokana na mwilingilino wa shughuli za Kiuchumi pamoja na

kuongezeka kwa wafanyakazi kwenye Viwanda, Biashara ndogo ndogo yapo makabila mengine yanayopatikana kibaha.

Aidha, Wazaramo ndio wanaochukua eneo kubwa la Halmashauri ya Mji Kibaha ambalo linahusisha Kata zote isipokuwa kata ya Msangani wakifuatiwa na Matumbi wanapatikana kwenye kata zote pia isipokuwa Kongowe. Hali kadhalika Wangindo

Makabila mengine yanayopatikana Kwenye Halmashauri ya Mji Kibaha ni wayao, Wamakonde, Wakwere, Wangoni, Wagogo, Wasukuma, Wanyamwezi, Wandengereko, Wamwera, Wachagga, Wapare na Wagweno

MTAWANYIKO WA IDADI YA WATU KWA JINSIA, UMRI NA MAKUNDI


Umri	Jinsi			Asilimia ya Jumla
	Me	Ke	Jumla	
0 – 14	22,305	22,537	44,842	34.9
15 – 29	18,684	21,743	40,427	31.5
30 – 49	14,586	14,453	29,039	22.6
50 – 64	4,639	4,209	8,848	6.9
65 +	2,439	2,893	5,332	4.1
Total	62,653	65,835	128,488	100.0

Chanzo: Ripoti II ya Sensa ya Watu na Makazi, 2012

Hata hivyo; Halmashauri ya Mji Kibaha ni halmashauri ya pili kwa kuwa na eneo dogo ndani ya Mkoa wa Pwani. Halmashauri inakadiriwa kuwa eneo lenye ukubwa wa Kilomita za Mraba 750. Katika eneo hilo hecta 17,490 zinatumiwa kwa Makazi na zinachangia 50% ya mapato ya ndani kwenye Halmashauri. Eneo hilo ni sawa na 23% ya Kilomita za Mraba 750 zinazotumika kwa ajili ya Mkazi na kuwa chanzo muhimu cha Mapato kwenye Halmashauri. Awali, Halmashauri ya Mji Kibaha ilikuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha.

MUUNDO WA KIUTAWALA

Halmashauri ya Mji Kibaha ipo chini ya utawala wa Kisheria, na imegawanyika katika tarafa mbili ambazo ni Kibaha na Kongowe, Kata Kumi na nne (14) ambazo ni Tumbi, Mailimoja, Kibaha, Visiga, Mkuza, Kongowe, Misugusugu, Picha ya Ndege, Msangani, Mbwawa, Pangani, Viziwaziwa, Tangini and Sofu. Aidha, Halmashauri ina Mitaa sabini na tatu (73)



Halmashauri ya Mji Kibaha, Mipaka ya Kata kutokana na Sensa ya Mwaka 2012